**Learning by Ear – Hygiene: How to avoid diarrhoea**

**Episode 05** **"Mito na Nyoka"**

**Author:** **Njoki C. Muhoho**

**Medical Advisor** **Dr Ng'ethe Muhoho**

**Editor** **Maja Braun**

**KISUAHELI** **ERIC PONDA**

| Scene | Characters | |
|---|---|---|
| 1 | 1. EDITH<br>2. MARIA | **SAM – 17, m.**<br>**EDITH – 40, f.** |
| 2 | 1. SAM<br>2. EDITH<br>3. MARIA<br>4. CHEMU<br>5. EDDI<br>6. NARRATOR | **MARIA – 43, f.**<br>**EDDI– 36, m.**<br>**DR SALLY – 34, f.**<br>**CHEMU – 15, f.**<br>**NARRATOR** |

**INTRO**

**MUSIC: THEME MUSIC**

**1. NARRATOR** **Hujambo na karibu kwa sehemu ya tano katika mfululizo wa vipindi vya Deutsche Welle, Noa Bongo Jenga Maisha yako, tukiwa bado tunazungumzia maada kuhusu Usafi na njia bora za kujikinga dhidi ya Ugonjwa wa Kuhara..Katika kipindi kilichotangulia , hatimaye Sam apelekwa hospitalini kwa wakati ufaao na kutibiwa dhidi ya ugonjwa huo wa kuhara.Kwa kweli Sam amenusurika. Kadhalika Daktari Sally apata muda wa kumuelezea Chemu na Sam kuhusu ugonjwa huu na chanzo chake.. Bara la Afrika halipaswi kuendelea kuwapoteza watoto zaidi. Kwani ni rahisi sana kuyazuia maradhi haya kuenea. Kadhalika matibabu ya haraka pia yanaweza kuepusha vifo zaidi miongoni mwa wanaoambukizwa.**

**Lakini zaidi jamii hii inahitaji kujifunza zaidi kuhusu ugonjwa huu. Endelea kuwa nasi ujifunze mengi kuhusu chanzo, tiba na kinga dhidi ya ugonjwa huu. Endelea kutega sikio uyafahamu yatakayowasibu Sam, Familia na Marafiki wake**.

## SCENE 1: PATH TO LOCAL RIVER

**2.** ***SFX: SOUNDS OF RIVER. COWS MOOING. CHILDREN PLAYING. NATURAL SOUNDS - BIRDS, WIND ETC.***

**3. MARIA** Edith,nifuraha iliyoje kurejea tena mahali hapa. Ni muda mrefu sasa tangu tulipoacha kuteka maji pamoja hapa mtoni.

**4. EDITH** **Najua hayo Maria .Lakini ni kwa vile nimekuwa na matatizo mengi nyumbani, ndio maana hujaniona hapa.Kwanza pigo la kumpoteza Mtoto wangu Fatu,kumuuguza Sam na kisha** … ***(sniffles like she is about to cry)***

**5. MARIA** **Nafahamu hayo yote swahiba. Kifo cha Fatu ni pigo kubwa na ndio sababu nilitaka tutoke angalau upunge upepo. Hilo litakusaidia.**

**6. EDITH** **Ama kwa hakika wewe ni rafiki wa dhati Maria. Japo mara nyingine huwa na vituko lakini bado ni rafiki wa kutegemewa.**

**7. MARIA** **Na hawa watoto wako wapi ? Walipaswa kuwa wametangulia. Natumai mvulana wako Sam anajichunga na msichana wangu Chemu!.**

**8. EDITH** **Usiwe mkali sana kwao rafiki yangu. Hawa ni watoto tu. Kwanza Sam anahitaji kumpumzika zaidi. Ameondoka Hospitalini siku mbili tu zilizopita.**

**9. MARIA** **Kweli , pia yeye anahitaji kupunga upepo.Sasa twende mtoni tukateke maji.**

**10. SFX:** ***SOUND OF COWS AND COWBELLS COMING CLOSE***

**11. EDITH** **Ahh, ni mambo gani haya?. Yaani tunapaswa kutumia maji haya pamoja na ngombe hawa.?**

**12. SFX:** ***SOUNDS OF CHILDREN PLAYING AND SPLASHING WATER GETTING LOUDER AS WELL***

**13. MARIA** **Hata si hawa ng'onmbe wanaonishangaza. Ni wale watoto pale.!**

**14. EDITH** **Nani? Sam na Chemu….., siwaoni..!**

**15. MARIA** **Hapana, hapana sio hao, ni watoto wale Edith…… huwaoni pale? Tazama wanafua**

**nguo zao, wengine wanaoga na hata kujisaidia kando kando ya mto.**

**16. EDITH** **Ohh kwani hawana akili timamu. Yaani wametoka kote huko kuja kujisaidia hapa mtoni? Kwanini wanafanya hivyo lakini?**

**17. MARIA** **Hivyo ndivyo mwanao Sam alivyokuwa akinisaidia kunyunyuzia shamba langu mbolea.**

**18. EDITH** Jamani **Maria, usiwe hivyo, humtendei haki mwanangu kwa kauli hizo!**

**19. MARIA** **Sawa ….sawa basi, sasa aidha tuwakanye au tusubiri hadi kinyesi hicho kitakaposombwa na maji ya Mto, ndipo nasi tuteke yetu ya kutumia..**

**20. EDITH** **Sasa unafikiri tutasubiri hapa kwa muda gani. Hebu tazama, ni wengi na wanazidi kumiminika mtoni.**

**21. MARIA** **Sawa … sawa… tuwakanye**.. ***(loud voice).***

***22. SFX: SOUNDS OF TWIGS BEING RIPPED OFF A BRANCH***

**23. MARIA** **Nyinyi ..nyinyi ….. ondokeni hapo!. Hamuoni tunayateka maji haya ya kunywa. Naja hapo, na nitakayemshika atakiona kilichomtoa**

**kanga manyoya… Nitawacharaza kwa fimbo hii hadi…hadi…. Wewe…!**

**24. EDITH** ***(laughing hysterically*) Ha ha ha… Maria wacha kunivunja mbavu kwa kicheko !**

**25. MARIA** **Nini kinachokufurahisha hapa? Hakuna cha kuchekesha ikiwa watoto wanajisaidia kwenye maji tunayotumia kunywa na kupikia!**

**PAUSE**

**26. MARIA** **Nafurahi kukuona ukitabasamu tena baada ya siku nyingi za majonzi. Ugonjwa huu wa kuhara kwa kweli ulikuharibia siha na hata tabasamu yako.**

**27. NARRATOR** **Bila shaka kuna sababu muhimu ya kinyesi kuwa na harufu mbaya. Kukiona au kusikia harufu yake tu huchafua roho. Mwanadamu anapasa kujitenga kabisa na uchafu unaotoka mwilini.Hiyo ndio tofauti iliyoko baina ya Mwanadamu na wanyama.**

**BRIDGE MUSIC**

**<u>SCENE 2 AT THE RIVER BANKS</u>**

**28. SFX:** ***WATER RUNNING. WATER BEING FETCHED WITH A SMALL CONTAINER AND REPEATEDLY EMPTIED INTO A SHALLOW MOUTH CONTAINER. NATURE SOUNDS.***

**29. SFX:** ***SOMEONE RUNS FAST. COMING CLOSER AND CLOSER***

**30. CHEMU** ***(screeming hysterically from far)*****Nisaidie…!, Edith nisaidie…. Nsaidieee…!**

**31. MARIA** **Ni msichana wangu Chemu..Chemu..Chemu.. naja… kuna nini?**

**32.** ***SFX: TWO SETS OF FEET RUNNING***

**33. EDITH Chemu… Sam yuko wapi? umemuacha wapi Sam.?**

**34. CHEMU** ***(Out of breath)*** **Nyoka .. Nyoka.. mkubwa.. nisaidieni…!**

**35. MARIA** **Nyoka? Hakuna Nyoka katika eneo hili… Yuko wapi, yuko wapi huyo nyoka unayesema?**

**36. EDITH** **Sam yuko wapi**

**37. CHEMU** ***(Crying)*** **Yuko na Sam.**

**38. EDITH** **Eti** ***Samu*** **yuko na Sam..kwani umepagawa?**

| | | |
|---|---|---|
| **39.** | **MARIA** | **Chemu, Sam yuko wapi? *(firmly)* huyo nyoka yuko wapi?** |
| **40.** | **CHEMU** | **Huyo nyoka yuko na Sam!** |
| **41.** | **MARIA/EDITH** | **Eti nini?** |
| **42.** | **CHEMU** | **Nyoka yuko na Sam!** |
| **43.** | **MARIA** | **Mungu wangu wee… Chemu hebu jieleze vizuri! tulia… tulia ….shusha pumzi kwanza..tena…haya tuambie kwa utaratibu Sam yuko wapi? Na nyoka huyo umemuona wapi?.** |
| **44.** | **CHEMU** | **Tulikuwa tukitembea na Sam na ghafla akasema tumbo lake linamsokota kisha akakimbia kichakani … ku.. ku.. ku..unajua,,,,,mara nikamsikia akipiga mayowe.** |
| **45.** | **EDITH** | Mayowe?**Kwa nini …? Halafu ikawaje?. Mwanangu Sam yuko salama.?** |
| **46.** | **CHEMU** | **Ghafla akatokwa na nyoka …alikuwa mwilini mwake… alikuwa …ooooh (Chemu screams).** |
| **47.** | **EDITH** | **Yuko wapi Sam?,,Umemuacha wapi?** |
| **48.** | **CHEMU** | **huyo….huyo …nyoka!** |

**49. MARIA Ooh Mungu wangu …hebu twende haraka tukamtafute…..!**

***50. SFX: FOOTSTEPS COMING CLOSER***

**51. SAM Msinitafute niko hapa…!.**

**52. EDITH Sam, mambo gani haya tunaambiwa kuhusu nyoka?**

**53. SAM Kuna vitu vinatoka tumboni mwangu vinafanana na nyoka.**

**54. MARIA Kijana umerogwa.. !... umerogwa? Chemu usithubutu ku..…**

***55. SFX: SOUND OF CAR DRIVING ON DIRT ROAD. IT STOPS***

**56. EDITH Tazama Shemeji yangu Eddi amekuja..**

**57. CHEMU Mjomba Eddi!!!**

**58. EDDI** Hamjambo nyote**? Kumbe hii hii ndio sababu nyumbani hakuna mtu?**

**59. MARIA Niliona ni vyema kunyoosha miguu pamoja na Mama Sam ili apunge upepo.Hata hivyo tulihitaji maji safi… kama kweli ni hivyo…**

**60. EDDI Sam, naona waendelea vizuri sasa..!.**

**61. MARIA** **Anaendelea vizuri…hana neno lakini bado hajapona kabisa . Akienda chooni anatoa vitu kama nyoka! Kwani ulimpa dawa za aina gani Hospitalini? Nilidhani munaelewa mnachofanya kama madaktari**

**62. EDDI** Anatoa nyoka..? Sam, una shida gani? Umenyamaza sana, unatatizo gani?

**63. SAM** Vitu ..vitu kama nyoka, vidogo vinatoka kutoka…. Kutoka … si unajua ni wapi…

**64. EDDI** ***(laughing)*** Usiwe na wasi wasi. Ni minyoo tu ya kawaida tumboni. Sasa imeanza kutoka baada ya kupewa dawa. Hiyo ni ile dawa aliyopewa hospitalini.

**65. MARIA** ***(shocked)*** Unamaana sasa mumeanza kuwapa watu minyoo.?

**66. EDITH** ***(crying)*** Uuui Uuuii, kwani mwanangu ameugua tena? Siwezi kustahamili ugonjwa tena katika familia hii.. siwezi ..!

**67. EDDI** Usiwe na wasi wasi Mama Sam. Sam si mgonjwa. Ugonjwa huu wa kuhara unasababishwa na vidudu kama vile amiba na vimelea. Hali hii husababisha Mtu kupoteza kiasi kikubwa cha maji mwilini na hata kufa. Lakini Sam yuko salama sasa.

**68. MARIA** ***(cynical)*** **Basi kwanini ametoa minyoo kutoka sehemu zake za nyuma. Huoni vile hawa watoto walivyotishika**?

**69. EDDI** Kwa kweli hakuna haja ya kuwa na wasi wasi. Sam alikuwa ameambukizwa ugonjwa huu pia ambao si nadra.Mayai ya chango hao yaliingia mwilini na yakaangua.Sasa baada ya kupewa dawa, minyoo wote wamekufa, na hawana nafasi ya kuendelea kuzaana tumboni. Ndio sababu pale Mtu anapokwenda kujisaidia nao wanapata njia ya kutokea.

**70. EDITH** Lakini ni vipi Sam aliweza kumeza minyoo hii? Lazima minyoo hii ilingia tumboni kupitia mdomoni mwake. Na katika nyumba hii watu hawali minyoo..

**71. MARIA** Eddi, Sasa unatukanganya, bora utufafanulie zaidi.

| | | |
|---|---|---|
| **72.** | **EDDI** | Nitafanya hivyo. Minyoo huingia tumboni kama mayai kupitia maji tunayokunywa au hata mboga na matunda. Na utumbo wa mwanadamu huwa sehemu muafaka wa mayai hayo kuendelea kuzaana. |
| **73.** | **MARIA** | Kwa hivyo Bw. Msomi, mayai haya huingia vipi kwenye mboga na matunda, maji na kadhalika... Nani hutaga mayai haya? |
| **74.** | **EDDI** | Sam, ni wapi na vipi uliweza kuona minyoo? Namaanisha minyoo iliyotoka tumboni mwako? |
| **75.** | **SAM** | Nilikuwa… nilikuwa…si unajua kisha… |
| **76.** | **CHEMU** | Alikuwa akijisaidia kichakani |
| **77.** | **EDDI** | **Sawa umepata jawabu.**! |
| **78.** | **MARIA** | Unaona, unaona Mama Sam, Nilikwambia nini kuhusu tabia ya mototo wako kwenda ku… ku… ku…sambaza mbolea katika mashamba ya watu? |
| **79.** | **EDITH** | Maria, wacha kumkemea mototo wangu... |
| **80.** | **MARIA** | Hata…. simkemei … nataka kuu… |

**81.** **EDDI** Sawa sasa nyamazeni nyinyi wawili… Mama Sam ulitaka kujua jinsi mayai haya yalivyoingia tumboni mwa Sam. Sasa kule kichakani alikokwenda kujisaidia ameacha mayai ambayo yanatosha kuwaambukiza wanakijiji wote ugonjwa wa kuhara na chango.

**82.** **SAM** Ohh samahani sana, si kutaka iwe hivyo… sikujua , tafadhali nisamehe…..

**83.** **CHEMU** ***(Kidding)*** Sam, wewe ni kama Kuku, tofauti ni kwamba mayai yako si mazuri... ni hatari…!

**84.** **EDITH** Tosha tosha enyi wawili inatosha . ***(To Eddi)*** Sasa tufanyej?

**85.** **MARIA** Najua ***(authoritatively),*** Sam, chukua jembe ukakizoe …..kinyesi chako… na ukitupe mahali kwengine mbali kabisa .

**86.** **EDDI** Wewe.. wewe … simakosa yake kwamba alipatikana na janga hili la kuambukizwa chango na vidudu vyengine. Hakujua kwamba kwa kufanya hivyo anahatarisha maisha ya wengine!

**87.** **MARIA** Sasa makosa ni ya nani? Hao madaktari pia wanapaswa kulaumiwa walitakiwa kumtibu apone kabisa.

**88.** **EDDI** Nina hakika kwamba Sam atapona kabisa. Minyoo hiyo sasa inatoka kwasababubu mazingira ya tumboni mwa Sam hayawezi kuwezesha minyoo kuendelea kutaga mayai . Inakufa sasa. La msingi ni tunalazimika kuuelimisha umma kuhusu suala hili.

**89.** **MARIA** Hasa wale watoto wenye tabia ya kujisaidia kando kando ya mto. Wale wenye mazoea ya kupeleka Ngombe kunywa maji na kufua mtoni na… Hata nashangaa hatujaanza kuhara.

**90.** **EDDI** Sasa mujue hivyo. Sote tumo hatarini. Mara nyingine sisi ni adui wa wengine. Na ndio sababu tunapaswa kujifunza njia bora za kujikinga.

**OUTRO:**

**91. NARRATOR** BADO KUNA MENGI YA KUJIFUNZA KUHUSU NJIA ZA KUSAMBAA UGONJWA WA KUHARA.INAVYONEKANA NI KWAMBA ZIPO NJIA BORA ZA KUEPUKA MARADHI HAYA IWAPO TU JAMII INAWAJIBIKA.EDDI AMEFAHAMU KWAMBA JAMII INAHITAJI KUHAMASISHWA ZAIDI NA KUPEWA ELIMU YA MSINGI KUHUSU KINGA.PIA SISI TUJIFUNZE MENGI ZAIDI KUHUSU SUALA HILI LA KINGA KATIKA MAKALA YAJAYO YA NOA BONGO.

IWAPO UNGEPENDA KUSIKILIZA TENA MAKALA HII, TEMBELEA MTANDAO WETU WA WWW.DW-WORLD.DE/LBE NA UKIWA UNA MAONI KUHUSU VIPINDI HIVI USISITE KUTUTUMIA . HADI WAKATI MWENGINE KWAHERI KWA SASA.